# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA SITA

**04 FEBRUARI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 04 FEBRUARI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

## III. MASWALI:

## OFISI YA WAZIRI MKUU:

**90. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali inatumia utaratibu gani wa kuratibu na kutekeleza ahadi za Viongozi Wakuu nchini ili zisionekane ni za uongo.

**91. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Mstaafu aliyecheleweshewa kupata mafao anaweza kudai fedha kutokana na usumbufu alioupata wakati anasubiri mafao yake.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**92. MHESHIMIWA ANTIPAS ZENO MGUNGUSI (MALINYI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatoa fedha za kukamilisha miradi ya Hospitali ya Wilaya ya Malinyi na Kituo cha Afya cha Ngoheranga.

**93. MHESHIMIWA REGINA NDEGE QWARAY (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Vifaa Tiba na Watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu.

**94. MHESHIMIWA TWAHA ALLY MPEMBENWE (KIBITI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, nini mkakati wa Serikali kusaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti kupata mapato kwa kuuza *Carbon Credit.*

## WIZARA YA NISHATI:

**95. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, upi mpango mkakati wa kufikisha nishati ya umeme kwenye maeneo yote ya uchimbaji wa Madini - Kilindi.

**96. MHESHIMIWA JACQUELINE KAINJA ANDREW (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itamaliza kusambaza umeme kwenye Vitongoji nchini.

**WIZARA YA MAJI:**

**97. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini miradi ya maji Wilayani Kyerwa itakamilika ili Wananchi wapate huduma ya maji.

**WIZARA YA KILIMO:**

**98. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, miradi mingapi ya umwagiliaji imepangwa kujengwa Wilayani Uvinza kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**WIZARA YA UJENZI:**

**99. MHESHIMIWA SHABANI OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi wa Barabara ya Mkuzi hadi Mlola kwa mkupuo mmoja kwa kiwango cha Lami.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**100. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, Serikali ina mkakati gani kwa kushirikiana na Serikali ya DRC kuanzisha usafiri wa kufika Lubumbashi kupitia Ziwa Tanganyika.

**101. MHESHIMIWA DKT. ANGELINE SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Wananchi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza watalipwa fidia zao kwa kuwa tathmini imefanyika mara mbili sasa.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**102. MHESHIMIWA OMAR ISSA KOMBO (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Nyumba za Polisi katika Kituo cha Polisi Micheweni.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**103. MHESHIMIWA DEODATUS PHILIP MWANYIKA (NJOMBE MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itachukua hatua za kuhakikisha uvunaji wa rasilimali misitu unazingatia uongezaji thamani.

**104. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, nini mpango wa Serikali kuondoa adha ya uvamizi wa Tembo katika Kijiji cha Nyabugombe Kata ya Nyakahura - Biharamulo.

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

**105. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuinua Lugha ya Kiswahili kupitia Vyombo vyake vya Habari vya Kitaifa.

**WIZARA YA FEDHA:**

**106. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Wawekezaji wa nje ambao kila baada ya miaka kadhaa hubadili majina ya Kampuni kwa lengo la kukwepa kodi.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**107. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE MLAGHILA JUMBE (KYELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi VETA Wilayani Kyela.

## IV. HOJA ZA KAMATI:

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA USTAWI NA MAENDELEO YA JAMII:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA AFYA NA MASUALA YA UKIMWI:**

Kwamba, Bunge sasa lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI kuhusu Shughuli za Kamati kwa Mwaka 2024.

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **04 FEBRUARI, 2025** | **KATIBU WA BUNGE** |